**JINA** …………………………………………………………………………………………
**RAKAMU**…………………………

**SAINI** ………………………………………………. **TAREHE** ……………………………

## MTIHANI WA PAMOJA

# Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari

**KISWAHILI KIDATO CHA NNE**

**KARATASI YA PILI 102/2**

**MUDA SAA2½**

**MAAGIZO**

(i) Karatasi hii ina sehemu nne. Ufahamu, Ufupisho, Matumizi ya lugha na Isimu-jamii.

(ii) Jibu maswali yote katika nafasi ulizoachiwa.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| UFAHAMU | 15 | |
| UFUPISHO | 15 | |
| MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**SEHEMU YA A : UFAHAMU (alama 15)**

1. **UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Ulimwengu unapaswa kuzua na mbinu za **kulitandarukia** tatizo ambalo linakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea, unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umaskini huu ni anuwai mathalan,ufisadi uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini, unaoathiri nchi fulani una athari pana sana. Uvunjifu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya **kuatika** maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa **kuyaburia madeni** mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umaskini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa

ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

**MASWALI**

a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea? (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umaskini? (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

d) Mfumo wa soko huru una madhara gani kwa mataifa machanga? (alama 2)

e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)

i) Kulitandarukia ……………………………………………………………………..

ii) Kuatika ……………………………………………………………………..

iii) Kuyaburia madeni ……………………………………………………………

**SEHEMU YA B: UFUPISHO: (Alama 15)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

**MUHTASARI [ALAMA 15]**

Katika nchi zilizoendelea, vijana wanapofikia wakati wa kumaliza masomo yao shuleni hujawa na mawazo mengi ya kazi watazozifanya. Huwa hawana hakika ni kazi zipi watapenda kuzifanya. Daima huwa wanafikiri na kubadili nia kuhusu jambo hili. Lakini wanapoendelea kukua kimwili na kiakili, huanza kufikiria kazi moja tu itakayowafaa na ambayo iko karibu na mahali wanapoishi.

Utafiti uliofanywa na wataalamu kuhusu maoni ya vijana umeonyesha kuwa vijana hawa baadaye hukata shauri kufanya kazi moja maalumu baada ya kusitasita mwanzo. Hufikiria uamuzi huo baada ya kugundua kuwa kazi watakazofanya zitakuwa ni zile zinazotegemea elimu yao na akili walizo nazo ingawa mwanzo fikira kama hizo walikuwa hawanazo.

Wanapoanza kazi viwandani na maofisini ndipo wanafahamu kuwa maisha ni tofauti kabisa na vile walivyokuwa wakifikiria walipokuwa wakisoma. Pia hugundua kuwa wasimamizi wao kama vile wanyapara katika viwanda ni watu tofauti kabisa na walimu wao wa shule. Wasimamizi hawa huwa ni watu wanaotaka kazi zifanywe bila uvivu wala uzembe. Hawa si wavumilivu kwao kama walivyokuwa walimu wao.

Mara nyingi wanafunzi wanaomaliza shule hufanya kazi kama zile za wazazi wao au jamaa zao. Wazazi wakiwa ni mafundi na wahandisi katika viwanda, wao pia hupendelea kazi hizo. Wasichana pia hupendelea kufanya vivyo hivyo. Hufanya kazi kama walimu, makarani, maofisini au wauguzi katika mahospitali.

Vijana hawa bila shaka huweza kufahamu kuwa hakuna kazi rahisi. Huwaona wazazi wao wanapotoka kazini na kujitupa vitini hoi na kujibarizi baada ya mchana kutwa au usiku kucha. Hapo basi huanza kuingiwa na akili za utu uzima. Siku yao ya kwanza katika kazi, vijana hawa hujiona wako katika hali ya ukiwa. Hawana wenzao waliokuwa nao shuleni.

Kila mmoja hujiona ni mgeni kwa mwenziwe. Baada ya muda mfupi kila mmoja wao hutulia katika kazi yake, ikiwa ni ya kutumia ubongo kama vile ukarani au ya sulubu kama vile ya kiwanda au mtambo. Pia huanza kupenda kazi yake ya maisha ikiwa hapatakuwa na hatari ya kuondolewa na kazi yenyewe kufungwa na wafanyikazi kupewa haki zao za kiinua-mgongo na malipo kama hayo.

(a) Kwa kutumia maneno kati ya 60 – 70, fupisha aya ya tatu za kwanza (alama 7)

**Matayarisho** *(mtiririko alama 1)*

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………….

**Nakala safi /Jibu**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………..…………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..…………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………..…………………………….

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….….

(b) Kwa kutumia maneno kati ya 55 – 60, fafanua changamoto zinazowakabili vijana wanapoajiriwa kazi.
(alama 6)

**Matayarisho** *(mtiririko alama 1)*

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….….

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….……

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….……

**Jibu**

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….………

**SEHEMU YA C: <u>MATUMIZI YA LUGHA</u>** (alama 40)

(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo:
(alama 1)

(i) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini ………………………………

(ii) Kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu ………………………..

(b) Andika neno lenye muundo wa sauti zifuatazo:
(alama 1)

Kipasuo sighuna cha midomo,irabu ya mbele kati tandazwa,nazali ghuna ya ufizi,kipasuo ghuna cha ufizi,irabu ya nyuma kati viringwa.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………….

(c) Unda neno lenye silabi mwambatano wa KKKI
(alama 1)

…………………………………………………………………………….

(d) Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiambishi `KU'
(alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(e) Unda Nomino mbili mbili kutokana na vitenzi hivi :
( alama 2)

(i) Kwea ……………………………………………

……………………………………………….

(ii) Pinda ……………………………………………….

……………………………………………….

(f) Tunga neno lenye mofimu zifuatazo;
(alama 2)

(i) Nafsi ya kwanza hali kanushi

(ii) Hali timilifu

(iii) Yambwa

(iv) Mzizi

(v) Kauli tendesha

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………

(g) Onyesha matumizi mawili ya parandesi. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

(h) Tunga sentens amrishi ukitumia kiwakilishi kiambata cha nafsi ya pili wingi.
(alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………….

(i) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo:
(alama 2)

Alinunuliwa mkate na mtoto wake.

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

(j) Iandike upya sentensi hii ukitumia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari.
(alama 2)

Mama <u>alimpokonya</u> mtoto wembe <u>mkali.</u>

.......................................................................................................................................................

…………………………………………………………………………………………………………………

(k) Andika sentensi hii katika wingi.
(alama 2)

Wenzo ukitumika gogo litasonga haraka.

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

(l) Huku ukitolea mfano mmoja mmoja onyesha miundo yoyote miwili ya ngeli ya LI - YA.
(alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………...

(m) Onyesha dhamira ya sentensi zifuatazo;
(alama 2)

(i) Fujo waliyozua ilisambaratisha mkutano wa kisiasa.

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………..

(ii) Mbona unamtesa mtoto hivyo?

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………..

(n) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi mwafaka cha <u>wakati</u>.
(alama 2)

(i) Maharusi walifunga ndoa,

(ii) Maharusi walienda Afrika Kusini kwa fungate.

………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………….

(o) Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 2)

Kwa sababu ya kutii kwake maisha ya mjini yalimwendea vibaya.

………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………….

(p) Iandike sentensi uliyopewa upya kulingana na maagizo.
(alama 2)

Ugonjwa wa malaria husababisha vifo vya watu wengi.

(Tumia kitenzi `FA' kauli ya kutendesha.

………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………….

(q) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mistari / mishale.
(alama 3)

Timu yao iliyotia fora sana ilituzwa tena.

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

(r) Bainisha yambiwa na kiima .
( alama 2)

Kijana hodari alimnunulia mnuna wake gari jipya kwa hundi.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(s) Bainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo;
( alama 3)

Mhalifu yu gerezani lakini anastahili kuachiliwa.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(t)Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kielezi.
(alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………

(u) Umaskini ni kwa ukata ,ujinga ni kwa …………………………………… na kijiji ni kwa

…………………………………..

(alama 1)

(v) Andika methali mwafaka inayotuonyesha kuwa ni vigumu kurekebisha mtu /jambo au hali iliyoharibika au isiyorekebika.
( alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………

**SEHEMU YA D: <u>ISIMU JAMII</u>** ( alama 10)

(a) Umepewa jukumu la kuwazungumzia vijana wenzako baada ya kukamilisha masomo ya shule ya upili kuhusu umuhimu kozi za kiufundi. Fafanua sifa zozote

tano za lugha utakayotumia.
(alama 5)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Eleza sifa zozote tano za sajili ya bungeni.
(alama 5)

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………